**HOTUBA YA MHE. SAIDI MECK SADIKI, MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO KATIKA MAADHIMISHO YA KILELE CHA SIKU YA WAUGUZI DUNIANI AMBAYO KIMKOA YANAADHIMISHWA WILAYANI ROMBO TAREHE 12/05/2017**

- Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Rombo;
- Ndugu Katibu Tawala Mkoa;
- Ndugu Mkurugenzi wa Halmashauri (W) Rombo;
- Ndugu Muuguzi Mkuu wa Mkoa;
- Ndugu Mwenyekiti wa TANNA Mkoa;
- Ndugu Wajumbe wa Sekretarieti ya Afya Mkoa;
- Ndugu Mganga Mkuu wa Mkoa na Waganga Wakuu wa Wilaya;
- Ndugu Wauguzi Wakuu wa Wilaya;
- Ndugu Wajumbe wa Sekretarieti ya Afya ya Hospitali ya Wilaya ya Rombo;
- Ndugu Viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali;
- Ndugu Viongozi wa Dini;
- Waandishi wa Habari;
- Wageni Waalikwa;
- Mabibi na Mabwana:

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika siku hii ya leo. Aidha nawashukuru Wauguzi kwa heshima kubwa mliyonipa ya kunishirikisha kikamilifu katika sherehe yenu ya kuadhimisha siku ya Uuguzi mkiungana na Wauguzi wenzenu pote duniani.

Nitumie fursa hii kuwashukuru kwa mapokezi mliyonipatia siku ya leo. Aidha, napenda pia kuwapongeza kwa maandalizi mazuri ya shughuli hii. Nafahamu kuwa mnao wajibu mkubwa wa kutoa huduma kwa wagonjwa waliopo katika vituo vya kutolea huduma

lakini, mmeweza kutekeleza maandalizi ya sherehe hii. **Hongereni Sana!**

**Ndugu Wauguzi;**
Aidha; napenda nitoe pongezi zangu za dhati kwenu kwa kuienzi siku yenu hii wakati mnaadhimisha kumkumbuka na kumuenzi mwanzilishi wa taaluma yenu ya Uuguzi ambaye alizaliwa miaka **197** iliyopita. Nawapongeza sana kwa kazi yenu nzuri mnayoifanya ya kuhudumia jamii kwa moyo pamoja na changamoto mbali mbali mnazokumbana nazo. Aidha natambua kuwa Muuguzi ndiye anayekaa na mgonjwa masaa mengi kuliko watumishi wengine wa afya. Kwa mantiki hiyo napenda kutoa wito kwa jamii itambue kuwa ninyi ni watu muhimu sana kwa jamii na kwa hakika mnastahili pongezi. **Hongereni Sana!**

Aidha, napenda kuwapongeza Wauguzi wote wa Mkoa huu kwa kukubali kufanya maadhimisho haya katika ngazi ya Mkoa. Ninazo taarifa kuwa, utaratibu huu ulianza mwaka 2016 ambapo maadhimisho haya yalifanyika katika Manispaa ya Moshi.

Nafurahi kuona utaratibu huu unaendelea na ndiyo maana leo tupo hapa Rombo katika kuadhimisha Siku ya Wauguzi katika Mkoa wetu. Napenda kutoa wito kwa uongozi wa TANNA na Muuguzi Mkuu wa Mkoa kuendelea kusimamia utaratibu huu. Suala hili ni muhimu kwani waswahili husema: **"Umoja ni Nguvu".** Mnapoungana hivi ni rahisi kushirikiana katika kujadili na kutafuta majibu ya changamoto mlizonazo kwa sauti moja.

**Ndugu Wauguzi;**
Nimefahamishwa kuwa, sherehe hizi za Wauguzi zinazoziadhimisha hapa leo zimeambatana na utoaji wa huduma mbalimbali bila malipo katika jamii yetu ya Wilaya ya Rombo.

Aidha, nafahamu kuwa, katika juma la mwisho la mwezi Aprili, 2017 hadi jana mmeweza kufanya yafuatayo:-

1. **Kutoa elimu ya unyanyasaji wa kijinsia kwa shule 09 za Sekondari zenye jumla ya wanafunzi 5,201 na kwa Shule za Msingi 05 zenye jumla ya wanafunzi 1,327:** Napenda kuwashukuru sana kwani tunalo tatizo kubwa katika Wilaya ya Rombo na Mkoa kwa ujumla katika suala la unyanyasaji wa kijinsia. Kwa mfano: kuanzia Januari,2017 hadi Machi, 2017, wanafunzi wapatao **163** wamepewa mimba katika Mkoa wetu kati ya hao wa sekondari **160** na shule za msingi **03** .Aidha Wilaya ya Rombo inaongoza kwa kuwa na wanafunzi **47 ikifuatiwa na Wilaya ya Same wanafunzi 46.**

    - Aidha, nitoe wito kwa viongozi ngazi ya Wilaya na Mkoa kuweka utaratibu wa kuendelea kutoa huduma ya kuelimisha jamii kuhusiana na mimba za utotoni. Nitoe wito kwa Jeshi la Polisi na viongozi wa Dini kutoa ushirikiano katika kukabiliana na tatizo la unyanyasaji wa watoto wetu pamoja na mimba za utotoni. Hata hivyo, lipo tatizo la wazazi na wanafunzi wa kike waliopewa mimba kutowataja wanaume waliowapa mimba na hii inafifisha juhudi za kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika.

2. **Kutoa elimu juu ya athari za ulevi uliokithiri pamoja na madawa ya kulevya:**

    - Ninazo taarifa kuwa, Wauguzi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali mmeweza kutoa elimu ya athari za ulevi na utumiaji wa madawa ya kulevya kwa jamii ya wana-Rombo. Nafurahi kusema kuwa elimu hii mmeitoa katika

kipindi muafaka kwani hivi sasa tunalo tatizo kubwa katika eneo hili la Rombo hasa kwa wananchi wa rika mbalimbali kujihusisha sana na ulevi uliopindukia pamoja na utumiaji wa madawa ya kulevya kama mirungi.

Napenda kutoa wito kwa wananchi kuachana na tabia ya utumiaji wa pombe uliokithiri kwani watalaamu wamefanya tafiti na kudhihirisha kuwa matumizi ya pombe yaliyokithiri pamoja matumizi ya dawa za kulevya na mirungi yana athari zifuatazo:-

(i) Kusababisha Saratani na magonjwa ya kuambukiza kama UKIMWI;
(ii) Kusababisha watoto kuzaliwa wakiwa na ulemavu wa akili;
(iii) Kusababisha kuvunjika kwa ndoa;
(iv) Kukosekana kwa nguvukazi na hivyo uchumi katika ngazi ya familia kuanza kudorora;
(v) Kutokana na ndoa kuvunjika jamii inajikuta kuwa na kundi kubwa la watoto wa mitaani.

3. **Aidha, nafahamu kuwa; Wauguzi mmefanikiwa kutoa huduma ya uchunguzi wa viashiria vya awali vya Saratani ya Mlango wa Shingo ya Kizazi.** Nimefahamishwa kuwa, wanawake wapatao **120** wamepatiwa huduma hiyo na waliopatikana kuwa na viashiria vya Saratani ni wawili **(02)** na waliokutwa tayari wana Saratani ni wawili **(02).**

Napenda kuwapongeza kwa mara nyingine tena kwa kuwa na ubunifu huu. Tumezoea kufanya sherehe kama hizi na hatukuwa na utaratibu kama huu. Utaratibu wenu umewezesha kuwa na matokeo chanya kwa wananchi, kwani wamefaidika moja kwa moja na hasa kwa kuchunguzwa afya

zao. Wakina Mama wanne **(04)** ambao wamepatikana kuwa na matatizo ya Saratani si haba ambazo sasa mtajua mapema jinsi ya kuwasaidia. Nitoe wito kwa wananchi kuendelea kutembelea vituo vya afya kwa ajili ya kupima afya zao. Tusisubiri mpaka hali iwe mbaya.

Wagonjwa wa Saratani, sasa wanaweza kupatiwa huduma ili kuokoa maisha yao.

**4.** Nafurahi kuwa Wauguzi mmeweza kuhamasisha wananchi kuweza kuchangia damu na tumeweza kupata damu kiasi cha lita **46** ambazo hakika zitaweza kuokoa maisha ya watu. **Ahsanteni sana** na naomba wananchi waendelee kutoa mchango wao wa kuchangia damu.

**Ndugu Wauguzi;**
Mmeeleza kuwa hadi sasa kuna jumla ya wauguzi na wakunga zaidi ya **30,000** hapa nchini na katika mkoa wa Kilimanjaro pekee kuna jumla ya Wauguzi **1,232.** Idadi hii imeendelea kupungua kutokana na Wauguzi **43** kupatikana na Vyeti Feki. Hiyo inathibitisha dhahiri ongezeko la wataaluma haliendani na ongezeko la watu na vituo vya kutolea huduma.

Hata hivyo, pamoja na upungufu huo, natoa wito kwenu kuwa; muendelee kutoa huduma iliyo bora na salama na si hivyo tu, bali muuthamini na kuheshimu uhai wa binadamu kwa kutoa huduma kwa haki bila kujali hali ya kiuchumi aliyonayo **mtu; rangi, kabila wala dini,** kama ambavyo mmerudia kiapo chenu hii leo. Ninajua kuwa wauguzi wengi wanafanya kazi yao vizuri kwa kufuata na kuzingatia maadili na misingi bora ya taaluma yao, lakini wapo wachache ambao wanataka kuichafua taaluma yenu kwa kwenda kinyume na maadili ya taaluma yenu. Natoa wito kwa viongozi, Wauguzi hao msiwafumbie macho.

Fanyeni jitihada za kuwabaini na kuwaelekeza na kama hawaelekei mamlaka za nidhamu zianze kuwachukulia hatua za kinidhamu ili iwe fundisho hata kwa wengine.

**Ndugu Wauguzi;**
Nimefarijika sana kuona maandishi katika mabango yenu yakisema **"Wauguzi wa Mkoa wa Kilimanjaro hatutavumilia vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga kwa uzembe, n.k.** Hakika nawapongeza sana kwa kuweza kuhamasishana juu ya hilo pasipo kujali uhaba wa wauguzi wataaluma ukilinganisha na idadi ya wateja mnaowahudumia pamoja na uzembe wa wataaluma wachache wakiwemo wauguzi kama nilivyosikia kwenye risala yenu. Ni kweli vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga katika Mkoa wa Kilimanjaro bado viko juu na sababu ya vifo vingi vinavyotokea zinaweza kuzuilika endapo wauguzi mtaamua kuwa makini sawasawa na ujumbe niliousoma kwenye bango lenu. Ninawaunga mkono katika kuitekeleza kauli mbiu hii. **Hongereni sana Wauguzi!** Hata hivyo, ipo haja kubwa kuendelea kuwahamasisha akina mama wazazi kutumia Kliniki ipasavyo.

**Ndugu Wauguzi;**
Nimezisikia changamoto mbalimbali zinazochangia kupunguza ubora wa utendaji kazi wenu. Moja kati ya hizo ambayo pia ndio inayoonekana kuwa kama tatizo sugu ni:

**Kwanza;** uhaba wa vitendea kazi. Napenda kuwatia moyo katika hili kuwa, Serikali yetu inao mpango kabambe wa utekelezaji wa huduma za afya. Mpango huu utapunguza kama sio kuondoa kabisa tatizo hilo.

Ninasema hivyo nikiwa na maana kuwa kwa kupitia mpango huu mtaweza kuainisha ninyi wenyewe kipi kitekelezwe kwanza na kipi kifanyike baadae kwa kushirikiana na timu zenu. Kadhalika kupitia mpango huo mtaweza kujiwekea utaratibu mzuri wa kutathmini utekelezaji wa mipango yenu.

**Pili;** kuhusu changamoto ya kuchelewa kupandishwa vyeo, napenda kuwajulisha kuwa, hali hiyo imetokana na zoezi la uhakiki wa wafanyakazi hewa pamoja na ninyi wenyewe watumishi kutojaza fomu za OPRAS kwa wakati. Aidha upandishwaji vyeo kwa kutumia OPRAS ulitakiwa kuanza tangu mwaka 2004 lakini wengi wenu mlikuwa bado hamjaanza kutekeleza hayo.

Nawaagiza ndugu Wauguzi jitahidini kujaza fomu hizo kwa wakati ili muweze kupandishwa vyeo kwa wakati, ukizingatia Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa **Dkt. John Pombe Magufuli** katika sherehe za Mei Mosi aliahidi kulitekeleza hilo katika mwaka wa fedha ujao na mara baada ya kukamilisha zoezi la kuhakiki watumishi wa Serikali.

Changamoto nyingine ni kuhusiana na kutolipwa posho kwa wauguzi wanaoingia zamu za usiku maana ni dhahiri kuwa masaa wanayofanya kazi ni sawa na kuingia zamu mbili. Niwaombe ndugu wauguzi muendelee kuwa wavumilivu huku tukiendelea kulifanyia kazi ombi hilo kwani hakuna asiyeona changamoto hiyo pamoja na wingi wa kazi anazokuwa nazo Muuguzi kwa siku.

**Ndugu Wauguzi;**

Kuhusu changamoto nyingine ya upungufu wa Wauguzi katika vituo vingi vya kutolea huduma nalo ni tatizo sugu ukichanganya na zoezi la uhakiki wa wafanyakazi hewa ambalo limeathiri pia Mkoa wetu kwa kiwango kikubwa.

Nimeshatoa maelekezo kwa waajiri kuomba kibali cha kuajiri. Kinachotakiwa kwa kila mwajiri kwa maana ya Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri na Ofisi yangu ni kuhakikisha kuwa wanaandaa mazingira mazuri yatakayowezesha kufanya watumishi watakaopangiwa wasikimbie au kutokuja kwenye ajira.

Aidha; mmesema kuwa wako baadhi ya waajiri wanaowashonea wafanyakazi **wao sare zinazofanana na sare za Wauguzi** (rangi nyeupe na blue), jambo hili hatutaliruhusu na ninatoa agizo kwa wafanyabiashara hao maana hata hapa rombo nimeambiwa wapo, waache mara moja na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Rombo ninakuagiza usimamie hilo. Vazi la wauguzi lina heshima yake kubwa na linapaswa kulindwa kwani Muuguzi ambaye hajavaa vazi hilo haruhusiwi hata kumhudumia mgonjwa wala kumshika.

**Ndugu Wauguzi,**
Mwisho; niwashukuru tena kwa maadhimisho haya na kwa kazi nzuri mnazozifanya kwa upendo na kwa kujituma pamoja na kuwa kunachangamoto kadhaa.

Nawatakieni nyote utendaji kazi mzuri na mafanikio mema katika kazi zenu.

**Asanteni Sana kwa Kunisikiliza!**